# HOTUBA YA IJUMAA

## مخاطر الطلاق

## Hatari za Talaka

**Imefasiriwa**

**Na**

**profesa/ Ayman Alasar**

Sifa njema zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mlezi wa viumbe vyote Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu: وَالصُّلْحُ خَيْرٌ {**Na suluhu ni bora**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninshuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mola peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake Mtume na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Uislamu umefanya maisha ya ndoa ni yenye utakatifu maalum na yenye nafasi tukufu, na kutengeneza haki na wajibu pamoja na adabu zinazosimamia utulifu wake mfungamano wake mshikamano wake na kudumu kwake katika wigo wa utulivu upendo huruma na kuheshimiana ambapo Anasema Mola Mtukufu:

وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ.

{**Na kaeni nao kwa wema**}. Na anasema Mtume S.A.W: “*Mbora wenu mbora wenu kwa familia yake*”.

Na mwenye kuzingatia ndani ya Quran Tukufu atakuta kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiita ndoa kuwa ni makubaliano mazito ili kuonesha wajibu wa kuiheshimu na kuchukuwa tahadhari kutokana na hatari ya kuibomoa na kuivunja, ambapo Mola Mtukufu Anasema: **وَأَخَذْنَ مِنكُم مِّيثَاقًا غَلِيظًا** {**Na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti**}.

Sharia ya Kiislamu imetoa wito kwa wanandoa wawili kila mmoja kumuangalia mshirika wa maisha yake kwa jicho la uadilifu na kuzingatia pande zenye kheir na kutazama hali bora ya kubakia maisha ya kifamilia yenye utulivu wa nafsi na furaha kwa kizazi, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ فَإِن كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَى أَن تَكْرَهُواْ شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيراً.

{**Na kaeni nao kwa wema, na ikiwa mmewachukia, basi huenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake**}. Na anasema Mtume S.A.W: "*Muumini wa kiume hamchukii Muumini wa kike, ikiwa atamchukia kitabia basi humridhia kwa upande mwengine*" kwani ukamilifu ni wa Mwenyezi Mungu peke yake, na kuzuiliwa kufanya makosa ni kwa Manabii wa Mwenyezi Mungu na Mitumie yake. Msemaji anasema:

*Na ambaye anaridhishwa na sifa zake zote --- inatosha mtu kuangalia kasoro zake*.

Katika mambo yasiyo na shaka ndani yake ni kuwa maisha ya ndoa yaweza kuwa na baadhi ya mitazamo ambayo inaweza pelekea utulivu wa kifamilia, kwa sababu hiyo tunakuta Quran Tukufu imeweka ufumbuzi wenye ufanisi na kuelezea kuwa kheiri yote ipo kwenye kuleta suluhu kukubaliana kuridhiana na kufanya wema, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

وَإِنِ امْرَأَةٌ خَافَتْ مِن بَعْلِهَا نُشُوزًا أَوْ إِعْرَاضًا فَلاَ جُنَاْحَ عَلَيْهِمَا أَن يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا وَالصُّلْحُ خَيْرٌ وَأُحْضِرَتِ الأَنفُسُ الشُّحَّ وَإِن تُحْسِنُواْ وَتَتَّقُواْ فَإِنَّ اللّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا .

{**Na mwanamke akihofia kutupwa au kutojaliwa na mumewe, basi si vibaya kwao wakisikizana kwa suluhu. Na suluhu ni bora. Na nafsi zimewekewa machoni mwake tamaa na choyo. Na mkifanya wema na mkamcha-Mungu basi hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda**}, ikiwa hali inahitaji kuingilia kati watu wa wanandoa miongoni mwa watu wenye mitazamo busara uzoefu wema na ucha-Mungu basi na iwe uingiliaji mzuri wenye nia ya

kujenga na kuondoa sababu za tofauti, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُواْ حَكَمًا مِّنْ أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِّنْ أَهْلِهَا إِن يُرِيدَا إِصْلاَحًا يُوَفِّقِ اللّهُ بَيْنَهُمَا إِنَّ اللّهَ كَانَ عَلِيمًا خَبِيرًا.

{**Na mkihofia kuwepo mfarakano baina ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa wa mume, na muamuzi kutokana na jamaa wa mke. Wakitaka mapatano basi Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye habari**}.

Katika hilo kuna malipo makubwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambapo Anasema:

لاَّ خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ إِلاَّ مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلاَحٍ بَيْنَ النَّاسِ وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتَغَاء مَرْضَاتِ اللّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا.

{**Hakuna kheri katika mengi ya wanayo shauriana kwa siri, isipo kuwa kwa yule anaye amrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu, basi tutakuja mpa malipo mkubwa**}. Na Mtume S.A.W anasema: “*Je nikupeni habari ya matendo yenye daraja kubwa zaidi ya ibada ya swala funga na kutoa sadaka? Maswahaba wakasema ndio, akasema Mtume S.A.W ni kusuluhisha kati yenu*”.

Ama ikiwa jambo limefikia kwenye dhana kuwa haiwezekani kuendelea maisha ya ndoa basi Sharia imetupa muongozo kutulia ili kimbunga kipate kutulia na nyoyo kulainika kusafisha nafsi na kutawala akili, kwani kutajitokeza hali ya kurudi nyuma na kurejea makubaliano ikiwa kuchunga kuendelea kwa familia.

********

**HOTUBA YA PILI**.

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee mbora wa viumbe Mtume wetu Muhammad pamoja na watu wake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa talaka hubomoa nyumba iliyoamrishwa na Sharia kujengwa kwenye misingi utulivu upendo na huruma, kama vile talaka inabeba hatari nyingi na athari mbaya kwa familia na kwa jamii, na hasa kwa upande wa watoto jambo linalosababisha matatizo ya kinafsi kijamii na hata kiuchumi na kupoteza msingi mizuri ya malezi na makuzi mema kwa sababu ya huo mpasuko wa kifamilia, jambo linalowafanya kuwa na hali ya matatizo ya kisaikolojia na kuchelewa kimasomo, na kufanya wepesi wa kuharibika kimaadili mwishowe kutekwa na kuingizwa kwenye makundi ya misimamo mikali matumizi ya nguvu na ugaidi, hivyo shetani anafanya kazi yake ya kupotosha wanandoa ili kubomoa familia, anasema Mtume wetu S.A.W: "*Hakika iblis huweka kitenda chake kwenye maji kisha anatuma jeshi lake aliyembora zaidi kwake ni yule mpotoshaji zaidi, ndipo anakuja askari wake na kumwambia nimefanya hili na hili, kisha iblis anasema kumwambia askari wake hujafanya chochote, kisha anakuja askari mwengine anasema sikumuacha isipokuwa baada ya kuhakikisha nimewaachanisha kati yake na mkewe, ndipo iblisi atakapo mkumbatia na kumwambia ndio wewe ndio umefikia lengo langu*". Jambo ambalo tunahitajika kuwa na uelewa na kuwa macho nalo pamoja na kufanya kazi ya kujifungua kwenye kamba za shetani.

Ni uzuri ulioje kuwepo makubaliano kuheshimiana na kupendana kati ya wanafamilia wote ili kufikia mshikamano na utulivu ndani ya jamii nzima.

**Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba Uunganishe nyoyo zetu na tufanyie vizuri mambo yetu**.